

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KIWIRA COAL MINE,
S.L.P 246,
KYELA-MBEYA.
11/01/2021

Kumb. Na. KCM/SS/JI/Vol. I/17

MWANAFUNZI

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA PAMOJA NA MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA
SEKONDARI KIWIRA COAL MINE KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA 2020.**

Ninafurahi kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021, **hongera sana!** Shule ipo umbali wa takribani kilometa 3 kutoka barabara kuu ya Kyela-Mbeya.

Muhula wa kwanza wa masomo utanza rasmi **tarehe 11/01/2021**, ambapo utatakiwa kuripoti siku hiyo kwa ajili ya kuanza ratiba za masomo kwa muhula. Hata hivyo mwisho wa kuripoti shuleni ni baada ya **siku saba (7) toka tarehe ya muhula wa masomo kuanza.**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

- a) Sare ya shule hii ni rangi ya damu ya mzee kwa suruali na sketi kama inavyoonekana kwenye kitambaa kilichoambatanishwa na fomu hii.
- b) Mashati mawili (2) rangi nyeupe ya mikono mifupi kwa wavulana na wasichana.
- c) Viatu pea mbili (2) vyeusi vya ngozi vyenye kamba
- d) Soksi nyeupe pea mbili (2) kwa wasichana.
- e) Soksi nyeusi pea mbili (2) kwa wavulana.
- f) Sare ya michezo ambayo ni traki suti ya rangi ya bluu bahari.

Zingatia:

- ❖ Wavulana hawatakiwi kushona suruali za kubana (modo)
- ❖ Wasichana washone sketi zinazovuka magoti.

VIFAA MUHIMU

- a) Daftari kubwa kumi (10) ambazo ni Kaunta buku Quire 3.
- b) Kalamu za wino za kutosha (Nyeusi au bluu)
- c) Mkebe wa hesabu
- d) Kamusi (Dictionary) moja ya kiingereza kwa kiingereza.
- e) Begi zuri au mkoba kwa ajili ya kubebea daftari

HUDUMA YA HOSTELI KWA WASICHANA

Shule ina huduma ya hosteli kwa wasichana, Hivyo mzazi au mlezi utakayependa mwanao akae hosteli fika shuleni au wasiliana na uongozi wa shule kwa maelekezo na ufafanuzi wa mahitaji ya wanafunzi wa hosteli

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii ni ya serikali na inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia na kutekeleza miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia Elimu nchini.

Uwapo shuleni, utatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa na kuelezwa hapa chini na pia utapewa nakala ya kujikumbusha mara tu utakapofika shuleni.

- a) Heshima kwa Viongozi, Walimu , wazazi, wafanyakazi wa shule wasio walimu,wanafunzi wenzako na jamii inayokuzunguka ni jambo la lazima.
- b) Kuhudhuria shuleni kila siku na kutekeleza yale yaliyopo kwenye ratiba ya shule.
- c) Kuwahi kufika shuleni, kutii na kufanya shughuli zote za darasani na nje ya darasa na nyinginezo utakazopewa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo kwa kipindi chote uwapo mwanafunzi wa shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mavazi yako, mwili wako na mazingira ya shule.
- f) Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote unaotakiwa.
- g) Ukigawiwa samani (kiti na meza) ni lazima ukitunze kikiharibika kwa uzembe utawajibika kulipa gharama au kutengeneza kipya

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana shuleni
7. Kuharibu kwa maksudi mali ya umma
8. Kudharau bendera ya taifa
9. Kuoau au kuolewa
10. Kupata mimba, kusababisha mimba na kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu itolewayo na Mwalimu.

MAMBO MENGINE MUHIMU

Pamoja na maelezo hayo hapo juu, naambatanisha.

Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi (Medical examination Form) kwenye hospitali ya serikali, ambayo baada ya mwanafunzi kupimwa matatizo au magonjwa yaliyorodheshwa, Mganga mkuu wa hospitali atajaza matokeo ya vipimo na itatakiwa kukabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara tu unapofika shuleni.

Mwisho, soma na zingatia maelekezo na maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KIWIWA COAL MINE SEKONDARI

MNG'ONG'O, J.M
MKUU WA SHULE
0755063232